

AZIMIO LA KIMATAIFA KUHHUSU HIFADHI ZA NYARAKA



Azimio lililopitishwa
na Kikao cha 36 cha
Mkutano Mkuu
wa UNESCO



Baraza ya Kimataifa la Hifadhi za Nyaraka

Hifadhi za nyaraka huhifadhi maamuzi, matendo na kumbukumbu. Nyaraka ni za kipekee na zisizo na urithi mbadala kutoka kizazi kimoja hadi kingine. Nyaraka hutunzwa kutokea kuundwa kwake ili thamani na maana yake vihifadhiwe. Ni vyanzo vya kuaminika vya habari ambavyo huimarisha uwajibikaji na uwazi katika hatua za utawala. Zina umuhimu mkubwa kwenye maendeleo ya jamii kwa kulinda na kuchangia kwenye kumbukumbu za watu binafsi na jamii. Upatikanaji wa wazi wa nyaraka huongeza ujuzi wetu wa jamii ya binadamu, hukuza demokrasia, hulinda haki za raia na huongeza ubora wa maisha.

Kwa maana hii, tunatambua

- **Uboora wa kipekee** wa nyaraka kama ushahidi halisi wa shughuli za kiutawala, kiutamaduni na kitaaluma, na kama picha ya mabadiliko ya jamii.
- **Umuhimu wa nyaraka** kwa ajili ya kusaidia ufanisi katika biashara, uwajibikaji na uwazi, kulinda haki za raia, kuanzisha kumbukumbu binafsi na za pamoja, kuelewa yaliyopita, kutunza kumbukumbu za sasa zitakazotumika kutoa mwongozo katika matendo ya baadaye.
- **Uanuwai wa nyaraka** katika kunakili kila nyanja ya shughuli za binadamu.
- **Miundo mbalimbali ya kuundia nyaraka** ikiwemo ya karatasi, dijitali, kusikia na kuona na mingineyo.
- **Jukumu la wahifidhi nyaraka** kama wataalam walio na elimu ya awali na endelevu, wanaotumikia jamii kwa kusaidia kuunda, kuchagua na kutunza nyaraka na kuhakikisha zinapatikana ili zitumiwe.
- **Uwajibikaji** wa pamoja kwa wahusika wote – raia, afisa jamii na waamuzi, wamiliki wa hifadhi za nyaraka za umma na za kibinafsi, wahifadhi nyaraka na wataalamu wa habari wengine - katika usimamizi wa nyaraka.

Kwa hiyo, tumekubaliana kushirikiana ili

- Sera na sheria sahihi za kitaifa kuhusu hifadhi za nyaraka zipitishwe na zitekelezwe.
- Usimamizi wa nyaraka uthaminiwe na utekelezwe kwa ufasaha na sekta zote binafsi au za umma ambazo zinaunda na zinatumia nyaraka kwa ajili ya kuendesha biashara zao.
- Rasilimali za kutosha zitengwe kwa ajili ya kusaidia usimamizi sahihi wa nyaraka, ikiwemo kuajiri wataalamu waliofuzu.
- Nyaraka zinasimamiwe na zihifadhiwe kwa njia ambazo zinahakikisha uhalisi, uaminifu, uadilifu na utumiaji wake.
- Nyaraka zipatikane kwa kila mtu, huku sheria zinazofaa na haki za watu binafsi, waanzilishi, wamiliki na watumiaji zikizingatiwa.
- Nyaraka zitumike kuchangia katika uhamasishaji kwa raia wawajibikaji.

Lilipitishwa katika Mkutano Mkuu wa Baraza la Kimataifa la Hifadhi za Nyaraka Oslo, Septemba 2010. Lilidhinishwa na Kikao cha 36 cha Mkutano Mkuu wa UNESCO, Paris, Novemba 2011.